JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Ofisi ya Rais
# Tawala za Mikoa
# na
# Serikali za Mitaa

# Uandaaji wa Mipango Shirikishi katika Ngazi ya Kijiji na Mtaa

# Utangulizi

Kijitabu hiki kinafafanua kwa lugha rahisi maana na hatua muhimu katika kuandaa na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa njia shirikishi katika ngazi ya serikali ya Kijiji, na ile ya Mtaa.

Baada ya serikali ya Tanzania kutambua umuhimu na ufanisi unaoweza kutokana na mipango ya maendeleo iliyozingatia dhana ya ushiriki, sera nyingi na hata baadhi ya sheria zimezingatia dhana hiyo. Kwa mtazamo huo, ngazi zote za serikali hasa zile ngazi za msingi, zinapaswa kutumia fursa hii ili kuboresha ufanisi katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo. Ili viongozi, wananchi na wadau wengine waweze kufaidika na dhana hii, ni vizuri basi maana ya dhana ya ushirikishwaji na mchakato mzima katika utekelezaji wake vikafahamika kwa wadau wa maendeleo katika ngazi ya msingi. Kijitabu hiki ni njia mojawapo ya kufikia lengo hilo.

# Maana ya Ushiriki na Ushirikishwaji

Maneno ushiriki na ushirikishwaji yamepewa maana nyingi na tofauti. Kuchangia katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa ama na viongozi au wafadhili mara nyingi kunaitwa ushirikishwaji. Vile vile kushiriki katika kuibua miradi, kupanga na kutekeleza kwa pamoja nako huitwa ushirikishwaji. Maana hii ya pili ndiyo hasa inayofaa kwa vile inawapa wananchi pamoja na viongozi wao fursa ya kutambua matatizo, kuweka vipau-mbele na kuibua mikakati ya utekelezaji wa pamoja. Pia inatoa fursa ya wadau kutoa maamuzi, au kwa maneno mengine, fursa ya kisiasa na ya kiutendaji. Hivyo basi kwa kuzingatia sheria za Serikali za Mitaa Tanzania, maana halisi ya ushirikishwaji ni ile inayotambua umuhimu wa fursa zote mbili ya kushiriki katika kufanya maamuzi na katika utekelezaji. Ushirikishwaji wa utekelezaji peke yake hautoshi.

Kwa hiyo wananchi, viongozi na wadau mbalimbali wanapaswa wajiwekee utaratibu wa kuhakikisha kuwa wanashiriki katika hatua zote mbili. Kwa vile serikali ya Tanzania inatambua umuhimu na mchango wa ushirikishwaji katika kupanua demokrasia na maendeleo endelevu, imetoa miongozo mbalimbali ya kuboresha ushiriki wa wananchi katika kupanga na kutekeleza miradi ihusuyo maendeleo yao. Ufuatao ni mchakato wa jinsi Serikali Kuu, Halmashauri, Kata, Vijiji na Vitongoji vinavyoshirikiana katika kuandaa na kutekeleza mipango shirikishi.

# Mchakato wa Mpango Shirikishi katika Serikali za Mitaa

Baada ya tafiti nyingi na majadiliano mbalimbali, serikali imeainisha mchakato maalumu wa kuandaa mipango shirikishi katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa. Mchakato huo una hatua tisa. Kila hatua inaonyesha nini kifanyike na mhusika wake. Ushiriki wa moja kwa moja wa wananchi upo zaidi katika hatua ya tatu na ile ya tano. Katika hatua ya tatu mwananchi anashiriki kutoa mawazo yake katika kuandaa mpango huo na anaweza kushiriki tena, kuupitisha mpango huo, katika hatua ya tano kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Kijiji, Kitongoji au Mtaa wake. Wananchi wanashiriki katika hatua nyingine kwa njia ya kuwakilishwa na viongozi waliowachagua, kama vile Mwenyekiti wa Kitongoji, Kijiji, Mtaa na Diwani.

Kwa ufahamu zaidi wa mchakato huo ufuatao ni muhtasari wa hatua hizo tisa.

## Hatua ya Kwanza

Wizara husika inatoa taarifa kwa Halmashauri juu ya kiasi cha fedha kitakachotolewa kwa Halmashauri kwa mwaka wa fedha husika. Fedha hizi zinapatikana kutoka kwenye fedha za maendeleo LGCDG yaani Ruzuku ya Maendeleo.

Ni vyema wananchi wakafahamu kuwa kila Halmashauri inastahili kiasi fulani cha fedha kama ruzuku ya maendeleo. Serikali Kuu hutoa ruzuku hiyo kwa kuzingatia vigezo kama vile:

- Uwezo wa Halmashauri husika katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo,
- Uwezo wa kuchangia fedha katika miradi,
- Uwezo wa kusimamia matumizi ya fedha hizo kikamilifu. Kwa mfano ni lazima Halmashauri husika iweze kuchangia asilimia 5 ya kiasi hicho cha ruzuku au gharama ya miradi itakayotekelezwa na fedha hizo.

Halmashauri ambazo zinashindwa kufaulu tathmini hiyo, hazipati ruzuku. Kukosa ruzuku kwa Halmashauri kunazikosesha pia Kata, Vijiji na Mitaa husika michango hiyo kutoka Serikali Kuu. Ni jukumu la Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Halmashauri kuziweka Halmashauri zao katika hali ya kustahili kupata ruzuku hizo.

## Hatua ya Pili

Halmashauri inatoa taarifa kwa Kata kuhusu kiasi cha ruzuku watakayopata kama mchango wa kutekeleza mipango ya maendeleo. Nakala za taarifa hupelekwa Serikali za Vijijini na Mtaa. Kimsingi asilimia 50 ya ruzuku ambayo Halmashauri imepokea inapaswa kupelekwa kwenye Kata, Vijiji na Mitaa ya Halmashauri hiyo. Wananchi kufahamu kiasi cha ruzuku watakachopata kutoka Serikali Kuu kunawawezesha kupanga mipango inayotekelezeka badala ya kupanga bila kujua wana uwezo kiasi gani. Wajibu wa kutoa taarifa hii ni wa Mkurugenzi wa Halmashauri husika. Hatua hii ya pili inaonyesha umuhimu wa mawasiliano katika Halmashauri na ngazi za msingi za Serikali ya Mitaa.

## Hatua ya Tatu

Serikali za Vijiji/Mitaa zinaandaa mipango yake kwa kutumia vikao mbalimbali na kwa kuzingatia kiasi cha fedha kutoka Halmashauri pamoja na michango ya wananchi na wadau wengine. Kimsingi wawezeshaji wa Halmashauri na Kata wanawasaidia viongozi na watendaji katika vijiji na mitaa kuhamasisha wananchi na wadau wengine kushiriki katika kuandaa mipango yao, na pia katika kuandaa mpango wa mwanzo (draft plan). Hatua hii inategemea utaalamu uliopo katika Kata na uwezo wake kushirikiana na viongozi na watendaji wengine katika kuwezesha mchakato shirikishi wa uandaaji wa mpango wa maendeleo. Ni vizuri pia kwa viongozi wa vijiji na mitaa wakatambua utaalamu uliopo kijijini kwao na kuutumia.

## Hatua ya Nne

Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) inapitia mipango ya awali (draft plans) ya Vijiji na Mitaa na kuainisha miradi inayohusu Kata nzima kama vile barabara, maji, elimu ya sekondari n.k. Vile vile KMK inakubaliana namna ya kugawa fedha ya ruzuku iliyoahidiwa na Halmashauri. Ni wajibu wa KMK kukubaliana juu ya vigezo vya kutumia kugawa fedha katika kutekeleza miradi mbalimbali. Shughuli hii ni muhimu sana na ndio maana KMK inapaswa kushirikisha wadau wote wa maendeleo katika Kata husika hususan asasi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini, sekta binafsi na makundi ya vijana na akina mama kama sheria ya Serikali za Mitaa inavyoagiza

## Hatua ya Tano

Mkutano Mkuu wa Kijiji husika unaandaliwa kujadili mipango kama ilivyoboreshwa na Kata. Ni Mkutano Mkuu tu ndio una madaraka ya kupitisha mpango shirikishi wa kijiji na bajeti yake kabla ya mipango hiyo kuwakilishwa kwa Halmashauri husika. Pamoja na kwamba wananchi walishiriki katika hatua ya tatu, ni vizuri washiriki pia katika hatua hii ili wachangie katika maamuzi ya namna ya kuweka vipaumbele na jinsi ya kuchangia na kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Malalamiko mengi ya wananchi juu ya michango wanayopaswa kutoa yanatokana na ushiriki wao mdogo katika kuamua kiasi, namna na wakati muafaka wa kutoa michango hiyo. Hatua hii ya tano inatoa fursa ya kupunguza tatizo hilo.

## Hatua ya Sita

Halmashauri husika inaandaa mpango wake kwa kuzingatia mipango ya vijiji. Mpango huo wa jumla unapitiwa na wataalamu, madiwani na baadaye kwenye mkutano wa Kamati ya Uratibu ya Mkoa (RCC) kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza la Madiwani kwa kupitishwa. Kama hatua hii itazingatiwa kwa ukamilifu, mipango au miradi iliyoibuliwa katika ngazi za msingi itapata nafasi pamoja na ile iliyoibuliwa na Halmashauri. Hii ni fursa ya kuunganisha masuala au maslahi ya Kitaifa, Halmashauri na vijiji na mitaa na vitongoji katika

mpango mmoja.  Hii ni mojawapo ya fursa muhimu ya kushirikisha Serikali Kuu, na ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa.

## Hatua ya Saba

Halmashauri inawasilisha mpango wake Wizarani kwa taarifa na kwa kupatiwa fedha za utekelezaji.  Muhimu katika hatua hii ni uwezo wa Halmashauri husika kuweka ripoti ya mpango katika hali nzuri ya kitaalamu na kuuwasilisha kwa wakati muafaka.

## Hatua ya Nane

Wizara ya Fedha inapitia mipango hiyo na inatoa fedha kwa Halmashauri husika.  Ni vizuri pia kwa Halmashauri husika kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa hatua hii.

## Hatua ya Tisa

Halmashauri husika kutoa taarifa kwa Kata, Vijiji na Mitaa juu ya kiasi cha fedha kilichopatikana ili utekelezaji wa miradi ile inayotegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu uanze.  Hii ina maana kwamba kutakuwa na baadhi ya miradi ambayo wananchi walishaanza kutekeleza kwa nguvu zao wenyewe, hivyo fedha hiyo ya ruzuku mara nyingi ni ya kuimarisha utekelezaji na isichukuliwe kuwa ndio pekee ya kutegemewa. Ieleweke kwamba upatikanaji wa taarifa juu ya fedha za ruzuku katika ngazi za msingi kutasaidia kuifanya jamii kuwa na ari ya kusimamia matumizi ya fedha hizo kwa ukamilifu.

## Mambo muhimu ya kuzingatia wakati Wananchi na Viongozi wanapoandaa Mipango Shirikishi ya Maendeleo

Pamoja na Serikali kuainisha hatua tisa za mchakato wa kuandaa na kutekeleza mipango shirikishi, kuna mambo muhimu sana katika kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa dhana hiyo ya mpango shirikishi. Tunafafanua baadhi ya mambo au misingi hiyo muhimu hapa chini.

### Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) kama kiungo muhimu

Kamati ya Maendeleo ya Kata ni kiungo muhimu kati ya Halmashauri na Vijiji au na Mitaa. Kazi kubwa ya KMK ni kuratibu mipango ya maendeleo katika vijiji au mitaa iliyoko ndani ya kata hiyo. Pia ni jukumu la KMK kuhakikisha kuwa vijiji au mitaa vinapatiwa taarifa muhimu na utaalamu wa kutosha kuwawezesha kuandaa mipango yao shirikishi na utekelezaji wake. Mojawapo ya taarifa muhimu ni ile ya kiasi cha fedha kitakachotolewa na Halmashauri kama mchango wake kwa vijiji na mitaa hiyo. Taarifa hii ni muhimu ili wananchi waweze kufuatilia matumizi ya fedha na kumhimiza Diwani wao ipasavyo.

### Asilimia 50 ya fedha za ruzuku ya maendeleo ni kwa ajili ya Ngazi za Msingi

Kimsingi asilimia 50 ya fedha zote za maendeleo zilizotoka Serikali Kuu (LGCDG) kwa Halmashauri zinapaswa kupelekwa katika ngazi za kata, vijiji na mitaa, kama mchango wa Serikali Kuu.

### Mipango ya Maendeleo lazima ianzie na kupitishwa na vikao vya kisheria

Serikali za Vijiji au Mitaa zinapaswa kuandaa mipango yao ya maendeleo na kuainisha bajeti ya utekelezaji. Mipango hiyo lazima ijadiliwe na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Hii ina maana kuwa mikutano ya kijiji ndiyo mhimili mkuu wa kuhakikisha kuwa wananchi wanashiriki kikamilifu katika kupanga na kutekeleza miradi yao. Kama vikao vya kijiji au mtaa havifanyiki, haiwezekani kuandaa mpango shirikishi.

## Vikao vya kisheria kama njia ya kufikia maamuzi

Vikao ni njia muhimu ya kufikia makubaliano au maamuzi ya pamoja. Vikao hivyo vya kuwezesha wananchi kushiriki katika mchakato wa kuandaa mipango shirikishi ni lazima vizingatie taratibu za kisheria hususan kutimiza akidi (quorum).

## Kuhusisha wadau wote:

Hii ina maana kuwa wadau mbalimbali wa maendeleo wajulikane katika ngazi ya kata, vijiji na mitaa na kushiriki kikamilifu. Matakwa yao na vipaumbele vyao lazima viheshimiwe. Kama wadau hawajulikani basi jitihada zifanyike ili waweze kutambulishwa na kushirikishwa katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo.

## Kusisitiza uwazi:

Ni vyema kama taarifa za vikao vya kuandaa mipango zitatolewa na kuwafikia wadau kwa muda muafaka ili waweze, sio tu kuhudhuria vikao hivyo, bali pia kujiandaa. Kwa mfano kutafuta taarifa na takwimu muhimu zitakazohitajika katika kuandaa mipango na kuibua miradi. Hivyo basi upatikanaji wa taarifa muhimu ni jambo la msingi katika kuandaa mipango. Kwa mfano bila taarifa kamili ya mapato na matumizi ya kata, kijiji au mtaa husika si rahisi kwa wadau kuandaa mpango shirikishi utakaotekelezeka.

## Kuwawezesha wananchi na viongozi

Kimsingi ni jukumu la Halmashauri au Kata husika kuhakikisha kuwa wananchi, na hasa viongozi wa ngazi ya kijiji, mtaa na kitongoji, wanapatiwa utaalamu wa kutosha ili waweze kushiriki kikamilifu na kuheshimu michango ya wadau wengine, katika kuandaa na kutekeleza mipango. Serikali inaamini kuwa wananchi wakiwezeshwa kiutaalamu, wanaweza kuongeza kasi ya maendeleo yao kwa sababu watakuwa na uwezo wa kuamua. Aidha mipango husika itakuwa imeanzia kwao. Ni vyema viongozi wanaochaguliwa, kuteuliwa au kuajiriwa wawe na sifa pamoja na elimu ya kiwango cha kutosha kwa kukamilisha shughuli hii.

## Uwajibikaji:

Kati ya faida zinazotokana na ushiriki wa wadau katika kuandaa na kutekeleza mipango, ni suala na uwajibikaji wa wadau katika utekelezaji. Mpango uliozingatia dhana ya ushirikishwaji kwa ukamilifu unatekelezeka kwa urahisi kwa vile wadau walishakubali na walishadhamiria (committed) sio tu maamuzi bali pia utekelezaji. Wadau wakiwajibika, viongozi hawatahitaji kutumia nguvu katika kufuatilia utekelezaji. Pia viongozi kueleza au kutoa taarifa muhimu hatua kwa hatua kuhusu miradi inayotekelezwa kutasaidia kuongeza hamasa kwa wananchi. Vilevile wananchi wataweza kuwawajibisha viongozi pale ubadhirifu au uzembe unapokwamisha ufanisi katika miradi.

# Hitimisho

Mojawapo ya mafanikio yanayotokana na maboresho ya Serikali za Mitaa ni kwamba Serikali nyingi za Mitaa zimeshaanza kuandaa mipango na kuitekeleza kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji. Aidha mafanikio katika kuboresha huduma za elimu ya msingi na ya sekondari, huduma za afya, upatikanaji wa maji na barabara yametokana na mipango shirikishi. Pia kamati mbalimbali zimeundwa na zinawawezesha wananchi kutoa michango yao sio tu katika kuboresha huduma bali pia wanapata fursa ya kushiriki katika maamuzi na utekelezaji wa maazimio yao. Kwa kiasi kikubwa mafanikio haya yanadhihirisha kuwa inawezekana kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia mfumo wa Serikali za Mitaa wa Tanzania . Changamoto kubwa ni jinsi ya kuyafanya mafanikio haya yawe ya kudumu na endelevu.

**Kijitabu hiki kimeandikwa kwa msaada wa maelezo kutoka katika kitabu kifuatacho:**

United Republic of Tanzania, President's Office, Regional Administration and Local Government, *Local Government Capital Development Grant System Planning Guidelines for Villages and Mitaa* October 2004

**PO-RALG**
Mlezi House
P. O. Box 1923
Dodoma
Tanzania
www.poralg.go.tz